SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

YALIYOMO

UZALISHAJI KWA MWAKA 2021.....5
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022.....8
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022.....9
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2021/2022.....11
CHANGAMOTO.....16
NJIA ZA KUTATUA CHANGAMOTO.....17
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA 2021/2022.....18
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO.....18
MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.....19
1. Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji.....21
PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU.....27
Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo.....30

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar.....32
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA KAZI ZA WIZARA.....33
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji.....34
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.....35
Programu Ndogo ya Uratibu naUtekelezaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili na Mifugo Pemba.....37
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....38
Makadirio ya Matumizi 2022/2023.....38
MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. 40
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO.....41
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.....43
65. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inaombewa jumla ya TZS. 2.464 bilioni kwa ajili ya ruzuku (TZS

846.500 milioni Mshahara, TZS 1.617 bilioni kwa matumizi mengineyo).....46
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI.....46
PL0102 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU.....47
Shabaha zitakazotekelezwa na programu ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu.....47
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.....54
UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA NA MBOGA, 2020 - 2021.....58

HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa Fedha wa 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa Rehma zake na kwa kutujaalia uzima wa afya pamoja na kuibariki nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Ni dhahiri kwamba amani na utulivu umezidi kuimarika kwa kipindi hiki chote chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, busara na uwezo zaidi wa kuiongoza Zanzibar na kuleta maendeleo makubwa.

3. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025. Tunazipongeza pia juhudi za Mheshimiwa Rais za kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za Serikali kupitia maagizo,

maelekezo, ziara zake na majadiliano ya ana kwa ana na watendaji wa Serikali. Hatua hizo zimeweza kuimarisha ufanisi katika utendaji, uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa majukumu ya Wizara na taasisi za Serikali.

4. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza viongozi wakuu wa kitaifa Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zao za kuhamasisha na kutoa miongozo katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi kwa umakini na umahiri wako wa kuliongoza vizuri Baraza hili la Wawakilishi. Chini ya uongozi wako Baraza hili limekuwa tulivu jambo ambalo limewafanya Wajumbe kuwa huru, kuchangia hoja na kutoa mawazo yao pasi na kikwazo kwa muda wote wa vikao vya Baraza. Vilevile nawapongeza Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati za Baraza la Wawakilishi nao tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

6. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kilimo, Biashara na Utalii chini ya

Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kufuatilia na kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2021/2022. Vilevile nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Abdalla Hussein Kombo, Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa miongozo na ushauri waliotoa kwa Wizara ya Kilimo katika kufanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2021/2022.

7. **Mheshimiwa Spika,** mwisho nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Micheweni kwa kunipa mashirikiano na kuwa pamoja katika suala zima la kufanikisha maendeleo ya jimbo letu na ya nchi kwa ujumla. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta maendeleo jimboni.

MIKAKATI YA KULETA MAGEUZI YA SEKTA YA KILIMO

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaendeleza Mipango na Mikakati iliyoanzishwa na Serikali katika kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inajitosheleza kwa mahitaji ya chakula. kwa kuendeleza kilimo biashara katika uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kuwawezesha vijana kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Juhudi nyengine kuimarisha uzalishaji wa mazao ya viungo, mboga na matunda pamoja na mazao ya mizizi

ambayo ndio chachu ya maendeleo katika sekta ya viwanda na kuendeleza uzalishaji wa zao la Nazi na Karafuu nchini. Vilevile upatikanaji mzuri wa huduma za mifugo ikiwemo dawa, chanjo na utoaji wa elimu juu ya ufugaji, uzalishaji wenye tija na matumizi ya mbegu bora za mifugo utaendelezwa. Mwisho Wizara pia itaendelea na usimamizi wa misitu ya hifadhi na ya jamii kwa lengo la kuhifadhi bioanuai, mazingira pamoja na kuimarisha huduma za utalii.

UKUAJI WA SEKTA YA KILIMO NA UZALISHAJI MWAKA WA FEDHA 2021/2022

9. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo (mazao, mifugo na misitu) inaendelea kuwa ni muhimili wa uchumi wa Zanzibar na inatoa mchango wa kujikimu kimaisha pamoja na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora. Jumla ya kaya 348,250 zilizopo Zanzibar zinajihusisha na kilimo, kaya 180,220 (asilimia 51.8) zinajihusisha na kazi za kilimo na kutoa mchango mkubwa katika nchi yetu (Zanzibar Statistical Abstaract, 2020 & Sensa ya Kilimo na Mifugo, 2019/20). Kwa mwaka 2021 Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 24.6 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 22.8 iliyoripotiwa mwaka 2020.

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa sensa ya kilimo ya mwaka 2019/20 kaya zinazojihusisha na kilimo zimeongezeka kutoka kaya 132,193 zilizoripotiwa mwaka 2007/2008 hadi kaya 180,220 mwaka 2019/20. Kati ya kaya 180,220 zinazojihusisha na kilimo, kaya

115,762 (asilimia 64.2) zinazojihusisha na mazao pekee, kaya 62,310 (asilimia 34.6) zinazojihusisha na mazao pamoja na mifugo, na kaya 2,149 (asilimia 1.2) zinazojihusisha na mifugo tu. Matokeo pia yameonesha eneo lenye ukubwa wa hekta 66,658 lililimwa mazao tofauti katika msimu wa vuli na hekta 59,356 zililimwa mazao msimu wa masika.

11. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaimarisha kilimo cha umwagiliaji maji ambapo eneo lote lililolimwa mazao msimu wa vuli, hekta 9,068 (asilimia 13.6), kwa upande wa msimu wa masika hekta 7,421 (asilimia 12.5). Aidha, takwimu zinaonesha eneo lenye ukubwa wa hekta 14,679 (asilimia 22.0) liliwekwa mbolea wakati wa mvua za vuli, ambapo eneo lenye ukubwa wa hekta 16,934 (asilimia 28.5) liliwekwa mbolea msimu wa masika. (Sensa ya Kilimo na Mifugo, 2019/20).

UZALISHAJI KWA MWAKA 2021

12. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kwamba jumla ya ekari 98,591 zimepandwa mazao mwaka 2021 ikilinganishwa na ekari 100,907 za mwaka 2020 tofauti ya ekari 2,316. Kati ya eneo hilo, ekari 82,121 (asilimia 83.3) zilipandwa mazao ya chakula, ambapo zao la muhogo lilichukua eneo kubwa la ekari 30,949 sawa na asilimia 31.4 ya eneo lote lilopandwa mazao mwaka 2021. Zao la pili lililotumia eneo kubwa la uzalishaji ni mpunga ambalo lilipandwa katika ekari 28,172 (asilimia 28.6). Aidha, ekari 16,470 (asilimia 16.7) zilipandwa mazao ya mboga. Eneo dogo kabisa la ekari 2,233

(asilimia 2.3) lilitumika kwa upandaji wa mazao ya jamii ya kunde. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha wakulima kwa kulima mazao ya jamii ya kunde, mboga, matunda na viungo ili kulitosheleza soko la ndani hasa kwa utalii sambamba na kuongeza kipato cha Taifa. **(Kiambatanisho Nam. 1A na 1B)**.

13. **Mheshimiwa Spika;** kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula umepungua kwa tofauti ya tani 12,584 kutoka tani 341,079 mwaka 2020 ikilinganishwa na tani 328,495 mwaka 2021. Upungufu wa uzalishaji umetokana na maeneo mengi kuwa hayakulimwa kutokana na kuendelea kwa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na vipindi virefu vya jua Unguja na Pemba. Aidha, uzalishaji wa mboga na matunda umeongezeka kwa tofauti ya tani 9,885 kutoka tani 54,935 mwaka 2020 hadi kufikia tani 64,820 mwaka 2021, kutokana na wananchi wengi kuhamasika na kilimo cha umwagiliaji. Vile vile, uzalishaji wa zao la muhogo umeongezeka kutoka tani 158,465 za mwaka 2020 hadi kufikia tani 181,668 mwaka 2021 na Viazi vikuu vimeongezeka kutoka tani 2,912 za mwaka 2020 hadi kufikia tani 7,746 mwaka 2021. Kwa upande wa zao la mpunga uzalishaji umepungua kutoka tani 40,328 mwaka 2020 hadi tani 30,353 mwaka 2021. **(Kiambatanisho Nam. 1A na Nam. 1B).**

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa zao la biashara la karafuu, takwimu zinatuonesha uzalishaji wa zao la karafuu umeongezeka kufikia tani 7,840.8 mwaka 2021

ikilinganishwa na tani 3,072.1 za mwaka 2020 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 155. Hali hii inatokana na kuwa na msimu mkubwa wa karafuu na juhudi za Serikali za utoaji wa miche ya mikarafuu bila ya malipo. Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa zao hili na kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora ya mikarafuu, elimu ya uoteshaji na uzalishaji. Aidha, Wizara inampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwapatia wakulima wenye kuyasimamia mashamba ya karafuu Hati za Matumizi ya Mashamba ya ekari tatu (3) Kisiwani Pemba. Hali hii, imeongeza ari na juhudi kwa wakulima ya kuotesha miche mipya ya mikarafuu pamoja na kuyasafisha na kuyatunza mashamba hayo.

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mazao ya mifugo takwimu zinaonesha kupungua kwa uchinjwaji wa Ng'ombe kutoka ng'ombe 29,844 mwaka 2020 hadi ng'ombe 25,916 mwaka 2021, Mbuzi/kondoo wamepungua kutoka 7,868 mwaka 2020 hadi mbuzi/kondoo 7,447 mwaka 2021. Aidha, uzalishaji wa Bata umeongezeka kutoka bata 1,660 mwaka 2020 hadi kufikia bata 3,193 mwaka 2021 na uzalishaji wa Kuku umeongezeka hadi kufikia kuku 751,073 mwaka 2021 ukilinganishwa na kuku 709,930 mwaka 2020. Vilevile, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai 12,024,496 (2020) hadi kufikia mayai 15,723,843 (2021) na maziwa kutoka lita 6,113,345 (2020) hadi kufikia lita 6,602,332. **(Kiambatanisho Nam. 1C na 1D).**

16. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya misitu, takwimu zinaonesha mwaka 2021 matumizi ya kuni yamepungua kutoka mita za ujazo 27,496 (2020) hadi mita za ujazo 25,813 (2021), sawa na asilimia 6.2. Matumizi ya boriti (majengo) pia yamepungua kutoka mita za ujazo 1,450 (2020) hadi 1,422 (2021) sawa na asilimia 1.93 Uzalishaji wa nguzo kubwa umepungua kutoka mita za ujazo 3,255 (2020) hadi kufikia mita za ujazo 3,098 (2021) sawa na asilimia 4.8. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kujengea umeongezeka kutoka mita za ujazo 2,878 (2020) hadi kufikia mita za ujazo 2,956 mwaka 2021 sawa na asilimia 2.7. Kwa ujumla matumizi ya nishati ya kuni yamepungua kutokana na juhudi inayochukuliwa na Wizara za kuhamasisha wanajamii katika uhifadhi misitu inayowazunguka na matumizi ya mbinu mbadala za nishati ikiwemo ya Gesi na majiko sanifu. **(Kiambatisho Nam. 1E).**

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022

17. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya 2030, Mipango Mikakati ya Kisekta ikiwemo Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ZASDP). Utekelezaji wa Mikakati hii kumesaidia kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wakulima hasa wa mazo

ya mboga, matunda na viungo jambo lililopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo.

18. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilitekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu Nne ambazo ni:
    1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
    2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu
    3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
    4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.
19. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Miradi (3) ya Maendeleo ikiwemo Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu katika mazao ya nafaka TANIPAC, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na Mradi wa Kudhibiti Nzi waharibifu wa Matunda.

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022

20. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS 4.00 bilioni kupitia vianzio vyake tisa (9) viliopo Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Wizara imekusanya Jumla ya TZS 3.160 Bilioni sawa na asilimia 79 ya makisio. **(Kiambatanisho Nam. 2A)**

21. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 53.70 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 17.18 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 12.62 bilioni Mishahara na TZS 4.56 bilioni matumizi mengineyo) na TZS 6.63 billioni ni Ruzuku (TZS 3.88 bilioni Mishahara na TZS 2.75 bilioni matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara iliidhinishiwa TZS 29.86 bilioni (TZS 23.88 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 5.98 bilioni kutoka SMZ).

22. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2021 hadi April, 2022 Wizara imepata jumla ya TZS 36.9 bilioni sawa na asilimia 69 ya fedha zilizoidhinishwa kati ya hizo TZS 9.70 bilioni zimetumika kwa matumizi ya kawaida (TZS 8.8 bilioni mishahara; TZS 851milioni matumizi mengineyo) Ruzuku ya TZS 3.6 bilioni (TZS 2.7 bilioni mishahara na TZS 927 milioni kwa matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Aprili, 2022 Wizara imepata TZS 23.66 bilioni ambapo TZS 21.6 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 2.0 bilioni kutoka SMZ **(Kiambatisho Nam. 2B)**

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2021/2022

23. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

1. Kukamilika kwa uchimbaji na ujenzi wa misingi ya saruji ya umwagiliaji yenye urefu wa mita 1,400 katika bonde la Mlemele. Aidha, uwekaji wa pampu katika visima 20 mabonde ya Cheju, Kibokwa na Kilombero umefanyika;

2. Jumla ya wananchi 325 (297 Pemba na 28 Unguja) wamelipwa TZS 934,467,900 ikiwa ni fidia kufuatia ujenzi wa mradi wa miundombinu ya umwagiliaji.

3. Ujenzi wa Tuta la kuzuia maji ya bahari kuingia katika eneo la kilimo huko Tovuni Pemba upo katika hatua za kukamilika kwa asilimia 95 kupitia Mradi Shirikishi wa Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi;

4. Wakulima 713 Unguja (wanawake 287 na wanaume 426 na wakulima 1,584 Pemba (wanaume 637 na wanawake 947) walipata fursa ya kutembelewa na mabwana na mabibi shamba na kupatiwa ushauri wa kitaalamu;

5. Wakulima 19,888 (Mradi wa Viungo 17,869; TAHA wakulima 1,350 na SOLIDARIDAD wakulima 666) walipatiwa mafunzo ya kupunguza upotevu wa

mazao, mbinu za kilimo bora na kilimo hai kupitia Miradi ya Kuendeleza Mboga, Matunda na Viungo;

6. Agizo alilolitoa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi huko Cheju la kuwapatia wakulima mbegu ya mpunga limetekelezwa ambapo tani 60 za mbegu ya mpunga (30 Unguja na 30 Pemba) aina ya SUPA, TXD 306, TXD 88 daraja la Certified 1 kutoka Agricultural Seed Agency, zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima.

7. Ujenzi wa Maghala ya kuhifadhia nafaka unaendelea katika eneo la Kizimbani Unguja (asilimia 48) na Ole Dodeani Pemba (asilimia 42).

8. Ekari 4,862 zimelimwa (Unguja 2,836 na Pemba 2026) na ekari 3923.5 zilizochimbuliwa na 478.50 zimeburugwa kupitia Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo;

9. Wizara inaendeleza juhudi za uzalishaji wa mazao ya viungo nchini kibiashara ambapo jumla ya ekari 65 zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha Vanilla (Vanilla International) ekari 10 kwa ajili ya mazao ya viungo mchanganyiko (TAHA) katika shamba la kilimo Bungi. Vilevile, Wizara imetenga eneo la ekari 7 Bambi kwa ajili ya majaribio ya kilimo cha pilipili hoho kwa kushirikiana na wazawa;

10. Jumla ya miche 511,427 ilioteshwa katika vitalu vya Serikali (410,850 Unguja na 100,577 Pemba)

ikiwemo ya Misitu, Matunda na Viungo. Aidha, Miche ya mikarafuu 104,300 (72,000 Pemba na 32,300 Unguja) na minazi 16,800 imeoteshwa;

11. Doria 243 (200 Unguja na 43 Pemba) zimefanywa katika maeneo ya rasilimali za Misitu ambapo matukio 45 yameripotiwa (25 Pemba na 20 Unguja) yaliyopelekea kesi 42 (18 Unguja na 24 Pemba). Kati ya kesi hizo 8 zimeripotiwa vituo vya polisi na 34 zimetatuliwa kwa mujibu wa sheria na kutozwa faini ya TZS 15.00 milioni;

12. Mizinga 200 ya kufugia nyuki wadogo wasiouma imetengenezwa na kugaiwa kwa wafugaji wa nyuki mizinga 50 kila Shehia za (Muungoni, Pangeni, Muyuni C na Kibele); pamoja na utoaji wa mafunzo ya kilimo hai kuhusiana na usarifu wa asali kwa wafugaji wa nyuki na wakulima 213 (110 Pemba na 103 Unguja) kupitia mradi wa ujenzi wa kituo cha Usarifu wa asali kwa fedha za UVIKO-19.

13. Watalii 16,085 walitembelea hifadhi za Misitu (Ngezi, Kiwengwa, Masingini na Jozani. Ambapo TZS 259,699,500/= Dola za Kimarekani 19,473 na Euro 1,020 zilikusanywa ikiwa ni ada ya uingizaji watalii;

14. Muongozo wa Uwekezaji kwa Misitu ya Hifadhi umetangazwa kupitia tovuti (www.utaliismz.go.tz) ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na magazeti ya hapa nchini;

15. Ng'ombe 381 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kimeta, chambavu ng'ombe 881 na mapele ya ngozi ng'ombe 100;

16. Wafugaji 5,444 (2,666 Unguja na 2,778 Pemba) wafugaji wa ng'ombe 3,062, mbuzi 1,257 na kuku 1,125 walitembelewa na kupewa ushauri juu ya ufugaji bora;

17. Jumla ya ng'ombe 256 (Unguja 183 na Pemba 73) wamepandishwa kwa njia ya sindano;

18. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo - ZALIRI kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine itatekeleza tafiti mbili Mpya zifuatazo:

a) Utafiti wa kupunguza kuenea kwa vidudu sugu vya magonjwa kwa kuchakata mbolea ya samadi ya kuku na

b) Utafiti wa kuongeza wigo wa kuchanja, usafi na usalama wa mabanda ya kuku katika kupunguza usugu wa madawa kwenye ufugaji kuku kibiashara;

19. Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa Uzalishaji wa Mazao ya Mboga na Matunda (Horticultural Strategy) umekamilika. Aidha, kwa sasa Wizara inaendele na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa Uzalishaji wa Mifugo, Mazao ya Viungo na uimarishaji wa zao la Karafuu nchini.

20. Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Mradi wa Agri-connect umefanikisha kongamano la Viungo

lililofanyika, Kisiwani Pemba na kuhudhuriwa na washiriki 150 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, likiwa na Maudhui ya kuimarisha Uzalishaji wa Viungo na kuweza kupenya katika soko la dunia, ambapo Vipaumbele 18 vimeibuliwa ili kufikia maudhui hayo;

21. Mapitio ya Sera ya Kilimo yamekamilika kwa ngazi ya Wizara; Sheria ya Minazi, Sheria ya Mbegu na Sheria ya Viuatilifu na Uhifadhi wa Mimea zimekamilika na kupitiaTume ya Kurekebisha Sheria zinaendelea na ukusanyaji wa maoni ya wadau;

22. Wizara ya Kilimo imetayarisha na kuwasilisha miradi 2 katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (Udhibiti wa Upotevu wa Mazao na Uendelezaji wa Miundombinu ya Umwagiliaji) yenye thamani ya Dola za Kimarekani 19,378,841;

23. Miradi miwili imetayarishwa kupitia fedha za Ahueni ya UVIKO-19 awamu ya pili ikiwemo mradi wa “uvunaji wa maji ya mvua kwa ujenzi wa mabwawa madodgo na ujenzi wa vituo vya huduma za sekta ya kilimo ki Wilaya;

24. Kupitia Miradi ya UVIKO-19 Wizara imetoa maeneo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo ikiwemo; Kibele hekta 65 ujenzi wa barabara za vijijini; Dunga hekta 63 eneo la viwanda; Konde ujenzi wa kituo cha dalaladala; Pujini hekta 10 na Kizimbani hekta 5 kwa ujenzi wa kituo cha Usarifu

wa asali; Kivunge kwa ujenzi wa kituo cha afya na Kidimni kwa ujenzi wa nyumba za kurekebisha tabia (Soba house);

25. Jumla ya TZS 5,600,000/ zimetumika kwa malipo ya likizo kwa wafanyakazi 56. TZS 2,01,265/= malipo ya ziada (overtime) na TZS 19,500,000/= kwa malipo ya ubani wafanyakazi 35; na

26. Kupitia mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNRMwinyi), Wizara imefanikiwa kuyapatia ufumbuzi malalamiko 72 kati ya 80 yaliyowasilishwa sawa na asilimia 90. Aidha, malalamiko 8 yanaendelea kufanyiwa kazi.

CHANGAMOTO

24. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a. Uwiyano mdogo baina ya wafanyakazi wataalamu wanaostaafu na wanaoajiriwa ilhali wataalamu wapo katika soko hawajaajiriwa;
b. Matukio ya uvamizi wa Maeneo ya hifadhi za misitu yameongezeka kwa kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu pamoja na makaazi;
c. Ubovu wa Mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen inayotumika kwa kuhifadhia mbegu za kupandisha ng'ombe kwa njia ya sindano;
d. Uvamizi wa maeneo ya mifugo yakiwemo Kisakasaka, Pangeni, vituo vya huduma za

mifugo Kama, Makunduchi, Mangapwani, Mtemwe, Ole, Konde na Micheweni; na

NJIA ZA KUTATUA CHANGAMOTO

a. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora tayari imekamilisha zoezi la uhakiki wa wafanyakazi, na ripoti imewasilishwa Serikalini;
b. Wizara inaendelea na jitihada za Kuhamasisha jamii katika uhifadhi wa misitu na inaendelea kuimarisha utalii kwa kuongeza vivutio vya utalii kwa lengo la kuwa na uhifadhi endelevu wa bioanuai na kuongeza kipato cha jamii na Taifa kwa ujumla. Wizara pia imeshaorodhesha na kukabidhi maeneo yote ya misitu ya jamii katika Mpango wa Taifa wa Benki ya Ardhi (Land Banking) kwa ajili ya hifadhi pamoja na kutafuta wawekezaji wa kuyaendeleza kwa faida ya nchi yetu;
c. Wizara katika bajeti yake ya mwaka 2022/2023 imetenga fedha TZS 650.00 Milioni kwa ajili za ununuzi wa Mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen inayotumika kwa kuhifadhia mbegu za kupandisha ng'ombe kwa njia ya sindano;
d. Wizara pia imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maeneo ya mifugo yakiwemo Kisakasaka, Pangeni, Nzi wengi kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za mifugo. Vilevile, Wizara imo katika hatua za kuyapatia hatimiliki maeneo hayo.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA 2021/2022

25. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Kilimo kupitia Programu zake kuu Nne (4) na ndogo Saba (7) ulikuwa kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

26. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilitekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu nne kama ifuatavyo:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu
3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo

27. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na utekelezaji wa Miradi mitatu (3) ya Maendeleo ikiwemo Mradi wa kudhibiti Nzi wa Matunda, Mradi wa kudhibiti Sumu Kuvu (TANIPAC) na Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na **(Kiambatisho Nam. 3A, 3B na 3C).**

MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

28. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara ya Kilimo, Uwagiliaji, Maliasili na Mifugo ilitekeleza Malengo yafuatayo:

1) Kujenga na kusimamia miundombinu ya Umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 370 katika bonde la Cheju "B'';
2) Kujenga uzio wenye urefu wa mita 1,500 katika mabwawa ya Umwagiliaji maji mabonde ya Chaani na Kinyasini.
3) Kutoa huduma za matrekta katika ekari 17,400 (Unguja 9,000 na Pemba 8,400) na kuhamasisha matumizi bora ya pembejeo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.
4) Ujenzi wa maghala mawili (2) ya hifadhi ya chakula yenye uwezo wa kuhifadhi tani 2000 kila moja, pamoja na chinjio la kisasa Kisakasaka
5) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 453 na kufanya matengenezo ya skimu nne za umwagiliaji maji katika maeneo ya Bumbwisudi na Cheju kwa Unguja na Saninga na Machigini kwa Pemba.
6) Kuhifadhi Misitu ya asili na ya jamii pamoja na kuimarisha shughuli za Utalii katika maeneo ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa na

kuendeleza uwindaji wa kitalii katika misitu ya jamii iliopo Mtende na Muyuni.

7) Kuotesha kibiashara miche ya Mikarafuu 500,000 Minazi 500,000 Misitu 800,000 na miche ya matunda na viungo 400,000;
8) Kutoa chanjo dhidi ya maradhi ya miripuko kwa ng'ombe 30,000; kuku 200,000 na mbwa 8,000 pamoja na kupandisha ng'ombe 2,000 kwa njia ya sindano
9) Kuendeleza tafiti za kisayansi 11 (9 Kilimo na Mifugo 2) zinazoendelea na tafiti saba mpya (3 Kilimo na 4 Mifugo) pamoja na tafiti 2 za kutatua changamoto za kijamii na kuimarisha miundombinu ya utafiti wa sekta ya kilimo;
10) Kutoa maslahi kwa Wafanyakazi 1,060, kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 20 na vijana 50 wanaondelea na masomo ya Udaktari wa mifugo nchini China pamoja na vyuo vyengine;
11) Kupitia Sheria 2 (Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999, Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996), pamoja na Kanuni 3 ikiwemo Misumeno ya Moto 2015, Uhifadhi wa Msitu ya Kimaumbile 2018 na Kanuni ya Ada na Tozo ya mazao ya Misitu 2013.
12) Kusimamia utekelezaji wa program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ZASDP;
13) Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu za Kilimo.

29. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo iliombewa jumla ya **TZS 37.30** bilioni ambapo kati ya hizo **TZS 5.15** bilioni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 2.86 bilioni Mshahara, **TZS 2.29** bilioni kwa matumizi mengineyo), **TZS 5.24** bilioni ikiwa ni Ruzuku (TZS 3.17 bilioni Mshahara, TZS 2.07 bilioni kwa matumizi mengineyo) kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Aidha, programu iliombewaTZS 26.90 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (TZS 23.885 kutoka EXIM BANK ya Korea na TZS 3.020 bilioni kutoka SMZ).

1. Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji

30. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 programu ndogo hii imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Ujenzi, usimamizi na ufuatiliaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji wa hekta 453 mabonde ya Cheju, Kilombero na Mlemele umefanyika kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa bwawa moja katika skimu ya Mlemele umekamilika.

ii. Ujenzi wa misingi mikubwa ya umwagiliaji maji kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa mita 13,700 (13.7km) mabonde ya Cheju na Mlemele umekamilika.

iii. Ujenzi wa barabara za mashambani zenye urefu wa 22.6 km kwa kiwango cha kifusi katika bonde la Kilombero umefanyika.

iv. Wananchi 325 (297 Pemba na 28 Unguja) wamelipwa TZS 934,467,900 ikiwa ni fidia kufuatia ujenzi wa mradi wa miundombinu ya umwagiliaji.

v. Uungaji wa umeme wa njia kuu unaendelea katika utekelezaji wake katika mabonde ya Cheju, Kilombero na Kibokwa ambapo jumla ya TZS 1,022,974,177 zimetumika.

b. Uimarishaji wa jumuiya za wakulima kwa kufanya mikutano 14 ya matayarisho ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa msimu wa masika mabonde 14 (8 Unguja na 6 Pemba) yakiwemo Mtwango, Cheju, Kibokwa, Mwera, Saninga, Mangwena, Ole, Dobi, Tungamaa na Kwalempona umefanyika. Aidha, maafisa ugani 29 wamepatiwa mafunzo juu ya taaluma ya uzalishaji wa mboga na matunda, upotevu wa mazao na udhibiti wa viwango vya chakula.

c. Jumla ya TZS 6.550 milioni zimetumika kwa ununuzi wa pampu yenye uwezo wa Horsepower 15 kwa ajili ya Kisima cha Cheju.

d. Uendelezaji wa kazi za uchimbaji wa visima 5 Cheju na ujenzi wa vibanda na uwekaji pampu kwa visima 20 katika mabonde ya Cheju, Kibokwa na Kilombero umefanyika.

31. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS 26.77 bilioni ambapo (TZS 616.7 milioni Mshahara, TZS 362.8 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 25.7 bilioni fedha za maendeleo (TZS 2.9 bilioni kutoka SMZ na TZS 22.8 bilioni kutoka kwa washirika wa

maendeleo EXIM BANK). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Programu imepata jumla ya TZS 23.87 bilioni sawa na asilimia 89 ya fedha zilizoombwa. Kati ya fedha hizo TZS 715.49 milioni mishahara na TZS 31.04 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 23.12 Bilioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS 21.16 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo EXIM BANK ya Korea na TZS. 1.96 Bilioni kutoka SMZ.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar

32. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Ukusanyaji wa taarifa za tafiti ulifanyika kwa mazao ya migomba na mboga. Aidha, eneo la utafiti wa maradhi ya umanjano wa mpunga “Rice Yellow Mottle Virus” (RYMV) liliwekewa mfumo wa umwagiliaji kwa njia ya matone pamoja na kupatiwa mbolea kwa urutubishaji wa ardhi.
2. Mbegu za viazi vikuu, mihogo, migomba zinaendelea kutunzwa na kuhifadhiwa.
3. Kazi za ufuatiliaji zilifanyika katika shamba la viungo na kuzungumza na wafanyakazi wa Kitengo hicho pamoja na watembezaji wageni na wasaidizi wao kwa ajili ya kutatuwa changamoto za ukusanyaji wa mapato.

33. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo iliidhinishiwa Ruzuku ya TZS 2.89 bilioni (TZS 2.33 bilioni Mshahara na 560.8 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 programu imepata jumla ya TZS 1.73 bilioni sawa na asilimia 60 (TZS 1.65 bilioni Mshahara na 80 milioni kwa matumizi mengineyo).

Programu Ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula

34. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a) Mbolea ya TSP tani 2.1 imeuzwa kwa TZS 2,100,000 na mbolea ya DAP polo 247 zimeuzwa TZS 14,850,000 na dawa lita 350 ziliuzwa kwa TZS 71,400,000 kwa jumuiya za wakulima;

b) Tani 146,076 za mazao ya kilimo kutoka na kwenda Tanzania Bara na nje ya nchi zimekaguliwa kwa lengo la kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu wa mazao. Mazao makuu yaliyokaguliwa ni ya nafaka (mchele, unga wa ngano, sembe, pumba, jamii ya kunde na nazi), mboga, viazi mviringo ambapo TZS 137,093,200 zilikusanywa kutokana na ukaguzi;

c) Kesi 4 za uingizaji mazao kinyume na sheria ziliripotiwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

d) Mabwana/mabibi shamba 40 walipatiwa taaluma ya utibabu wa mimea na wameweza kuwafikia wakulima katika maeneo ya Unguja na Pemba,

pia wakulima **27** walijengewa uwezo juu ya mbinu mchanganyiko za udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu.

e) Wakulima 1,860 (wanawake 1,112 na wanaume 748) walipata fursa ya kutembelewa na mabwana na mabibi shamba. Aidha, vikundi vipya 21 (kila kikundi kina watu 18) vinavyojumuisha wakulima 360 (6 Pemba na 15 Unguja) vya uzalishaji wa mazao ya mboga, matunda na viungo (tungule, vanilla, pilipiliboga, nanasi na tangawizi), zimepatiwa mafunzo kupitia mashamba darasa kwa kushirikiana na Jumuia zisizo za kiserikali za miradi ya mboga na matunda, Community Forest Pemba (Mradi wa viungo), UWAMWIMA, TAHA, Feed the Future na Solidaridard.

f) Uhamasisha wawekezaji katika uzalishaji wa mazao ya kimkakati ikiwemo mpunga, mboga na matunda, mazao ya viungo na miwa unaendelea. Vikao vilifanyika baina ya Uongozi wa Wizara, wafanya biashara wa pembejeo wakulima wa miwa na uongozi wa Shirika la Sukari Mahonda kwa lengo la kuwajulisha wahusika juu ya uamuzi wa Serikali kusimamisha taratibu za kutoa pembejeo kwa njia za ruzuku na kuhamasisha kilimo cha miwa kwa njia mikataba.

g) Taaluma za kilimo hai kwa mazao ya mboga, matunda na viungo, imetolewa kupitia BEOs na

wakulima kwa kushirikiana na Taasisi za kiraia zikiwemo TAHA, UWAMWIMA, International Institute of Biological Agriculture na jumla ya wakulima 3,372 wamefikiwa.

h) Utekelezaji wa mradi wa udhibiti wa nzi wa matunda umeanza kama unavyoonekana **(Kiambatisho Nam.3A).**

35. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu iliidhinishiwa TZS 5.28 bilioni kati ya hizo TZS 4.69 ni kwa matumizi ya kawaida (TZS 2.24 bilioni ni Mishahara na TZS 1.92 bilioni kwa kazi za kawaida), kwa fedha za Maendeleo ni TZS 1.15 bilioni (TZS 100 milioni kutoka SMZ na TZS 1.05 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia mwezi April, 2022 programu imepata jumla ya TZS 2.29 Bilioni sawa na asilimia 43 (TZS 1.98 bilioni ni Mishahara na TZS 143 milioni kwa matumizi mengineyo), kwa fedha za Maendeleo ni TZS 165 milioni ambapo TZS 112 Milioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 53 milioni kutoka SMZ.

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

36. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Matrekta 28 (Unguja 18, Pemba 10) yamefanyiwa matengenezo madogo na yanaendelea na kazi za ukulima. Aidha, ukarabati wa jengo moja la ofisi pia umefanyika;
2. Ekari 4,862 (Unguja 2,836 na Pemba 2026) zimelimwa. Zilizochimbuliwa ni 3923.5 na zilizoburugwa 478.50
3. Matrekta 26, Majembe ya kuchimbia (Disc Ploughs) 27 na majembe ya kuburugia (Disc harrows) 23 ya yamefanyiwa ukaguzi Unguja. Aidha, matrekta 14, majembe ya kuchimbia 14 na majembe ya kuburugia 8 yamefanyiwa ukaguzi Pemba.
4. Jumla ya TZS 413,898.818 zimetumika kwa kulipia deni la matrekta ya Mahindra kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

37. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS 2.35 bilioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 842.3 milioni ni mshahara na TZS 1.51 bilioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 programu imepata jumla ya TZS 1.35 bilioni sawa na asilimia 57 (TZS 581.3 milioni Mishahara na TZS 767.5 milioni kwa matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

38. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu inatekelezwa kupitia programu ndogo ambayo ni:

Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu;

Programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu

39. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Jumla ya miche 511,427 (410,850 Unguja na 100,577 Pemba) ilioteshwa katika vitalu vya Serikali ikiwemo (Misitu 400,430 Matunda na Viungo 111,267);

2. Hekta 3 (1 shamba la Chaani na 2 Dunga-Jendele) zilipandwa miti ya misitu. Aidha, hekta 25 (8 Unguja Ukuu Kaepwani, 1.5 Makoba, 4.5 Chukwani, 5 Charawe, 3 Gando na 3 Tumbe Magharibi) zimerejeshewa kwa kupandwa mikoko kupitia Kamati za Uhifadhi na Miradi ya TASAF;

3. Wafugaji 26 (16 Wanaume na 10 wanawake) walipatiwa mafunzo ya kugawa nyuki wadogo kwa lengo la kuongeza nyuki hao. Wafugaji 375 (240 Unguja na 135 Pemba) walifanyiwa tathmini ya uzalishaji wa asali. Vile vile, Vibanda 5 na Mizinga 200 ya kufugia nyuki wadogo wasiouma iligawiwa kwa wafugaji wa nyuki kupitia mradi wa ICIPE. Aidha, tani 5.358 (2.896 Pemba na 2.462 Unguja) za asali zimezalishwa.

4. Miradi saba (7) ya uwekezaji imeibuliwa na kutangazwa ili sekta binafsi ziweze kuomba kuekeza. Hata hivyo, Idara imeendelea na kushajiisha Kampuni za kutembeza Watalii, ambapo Jumla ya watalii 31,371 walitembelea hifadhi za Misitu (Ngezi,

Kiwengwa, Masingini na Jozani). Aidha, kati ya watalii hao 28,923 (6,496 wa ndani na 22,427 wa nje) walitembelea hifadhi za Unguja na watalii 2,448 (2,300 wa ndani na 142 wa nje) walitembelea hifadhi ya Ngezi – Vumawimbi na kuchangia mapato yaliotokana na ada za viingilio TZS 259,699,500 Dola za Kimarekani 19,473 na Euro 1,020;

5. Mikataba 22 ya usimamizi wa Misitu ya Jamii imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu. Kati ya hiyo 11 ya zamani iliyopitiwa upya na 11 mipya ikiwemo ya Shehia za Kibondeni, Kigunda Muanda, Fujoni, Tumbatu, Kikungwi, Mzuri Kae, Makoongwe, Wambaa, Pujini na Shamiani. Aidha, Mkataba wa Biashara ya hewa ya Ukaa kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Shirika la Kimataifa la TERAGLOBAL umeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupitiwa;

6. Doria 243 (200 Unguja na 43 Pemba) zimefanywa katika maeneo ya rasilimali za Misitu ambapo matukio 45 (25 Pemba na 20 Unguja) yaliyopelekea kufunguliwa kwa kesi 42 (18 Unguja na 24 Pemba). Kati ya kesi hizo (8 zimeripotiwa Vituo vya polisi na 34 zimehukumiwa kwa mujibu wa sheria baada ya watuhumiwa kukiri makosa TZS 15 milioni. Aidha, Misumeno ya moto 22 (15 Pemba na 7 Unguja) iliyotumika bila ya ruhusa imekamatwa kuhifadhiwa ghalani kwa lengo la kuangamizwa.

7. Matayarisho ya tathmini ya kutambua idadi ya Wanyama adimu katika maeneo ya msitu wa Vundwe, Pengeleni na Nongwe ambayo yamekusudiwa kupandishwa hadhi kuwa Msitu wa

hifadhi yamekamilika na tathmini imepangwa kufanywa mwezi Machi 2022.

40. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Misitu iliombewa jumla ya TZS 2.76 bilioni ambapo (TZS 2.24 bilioni Mshahara na TZS 521.195 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Programu imepata jumla ya TZS.1.5 bilioni sawa na asilimia 54 (TZS. 1.43 bilioni Mishahara na TZS.62.4 milioni kwa matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

41. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Mifugo ina jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake. Programu inajumuisha Programu Ndogo Moja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar.

Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo

42. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Ng'ombe 256 (Unguja 183 na Pemba 73) wamepandishwa kwa njia ya sindano;

2. Jumla ya ng'ombe 724 (Unguja 432 na Pemba 292) wamepandishwa kwa njia ya sindano. Lengo la upandishaji ni kupata ng'ombe bora wa maziwa kwa ajili ya kuzalisha maziwa ya kutosha na yenye ubora;

3. Jumla ya ng'ombe 381 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kimeta na chambavu, ng'ombe 881 na mapele ya ngozi ng'ombe 100. Kuku 75,265 (Unguja kuku 66,120 na Pemba kuku 9,145) kuku 50,446 dhidi ya ugonjwa wa mahepe (New Castle Disease) kuku 18,758 ugonjwa wa Gumboro, kuku 5,261 ugonjwa wa ndui (Fowl Pox) na 800 Mareck's.

4. Mbwa 8,023 (Unguja 6,225 Pemba 1,798) walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa (Rabies). Uchanjaji kwa wanyama ni kudhibiti maradhi ya miripuko yasisambae na kuleta madhara kwa binadamu na wanyama. Hapa Zanzibar.

5. Mbwa 49 na paka 120 wamefugwa kizazi ili kupunguza idadi ya mbwa na paka wazururaji. Mbwa na paka wanaozurura ni sababu moja wapo ya kuwepo kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa hapa Zanzibar.

6. Wafugaji kuku 185 (165 Unguja na 20 Pemba) walipewa mafunzo juu ya ufugaji bora wa kuku kutoka katika Wilaya ya Mjini – 5, Magharibi

"A" – 31, Magharibi "B" – 27, Kaskazini "A" – 37, Kaskazini "B" – 25, Kati – 40 na Micheweni – 20, Pia wafugaji wa ng'ombe wa maziwa 22 kutoka Wilaya ya Kati walipewa mafunzo ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa. Mafunzo hayo yanahusu upandaji wa malisho, usafi wa mabanda, kiwango cha ulishaji, lishe ya chakula na kukinga maradhi mbali mbali ya mifugo.

43. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo iliombewa jumla ya TZS 5.29 bilioni ambapo kati ya hizo TZS 2.32 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.63 bilioni mshahara na TZS 695.34 matumizi mengineyo). Aidha, programu iliombewa TZS 1.70 bilioni kwa kazi za Maendeleo kutoka SMZ kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Chinjio la Kisasa Kisakasaka. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Programu imepata jumla ya TZS.1.37 bilioni sawa na asilimia 26 (TZS. 1.3 bilioni Mishahara na TZS.60.1 milioni kwa matumizi mengineyo).

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar

44. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a) Tafiti nne (kuku, mbuzi, kupe na majani) zinaendelea kutekelezwa hatua tofauti;

b) Ekari 3 (Unguja 2 na Pemba 1) kwa ajili ya

mbegu za malisho zimepandwa halkadhalika tumetoa mbegu kilo 285 kwa wafugaji.

c) Ujenzi wa jengo la kiwanda cha chakula cha kuku umefika asilimia 70, kwa upande wa maabara pamoja na ujenzi wa mabanda matatu ya utafiti wa Ng'ombe, Mbuzi na Sungura unaendelea.

45. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, iliombewa Ruzuku ya TZS 1.39 bilioni (TZS 706.30 milioni Mshahara, TZS 685.40 milioni kwa matumizi mengineyo). Vilevile, Taasisi iliombewa TZS 1.26 kutoka SMZ kwa kazi za Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa majengo ya Taasisi Unguja na Pemba). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 programu imepata jumla ya TZS 546.1 Milioni sawa na asilimia 39 ambapo (TZS 466.1 milioni ni mshahara na TZS 80 milioni kwa matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA KAZI ZA WIZARA.

46. Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi wa sekta za kilimo.

Programu imegawika katika program ndogo tatu:

a. Programu ya Utawala na Uendeshaji;
b. Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti;
c. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Kazi za Kilimo Maliasili na Mifugo Pemba.

Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji

47. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1 Jumla ya TZS 5,600,000/ zimetumika kwa malipo ya likizo kwa wafanyakazi 56. TZS 2,01,265/= malipo ya ziada (overtime) na TZS 19,500,000/= kwa malipo ya ubani wafanyakazi 35;

2 TZS 18,370,000/= malipo ya viza kwa wanafunzi 12 waliopo nje ya nchi na vitabu wanafunzi (43) waliopo nje na ndani ya nchi. TZS 8,621,500/= wamelipwa wafanyakazi (9) waliopo masomoni katika fani za Irrigation engineering, Agriculture and community development, Bio-technology and Laboratory science. TZS 3,000,000 milioni zimetumika kwa mafunzo elekezi kwa wafanyakazi 20 na TZS 2,155,885 malipo ya kufanya kazi kwa muda wa ziada.

3 Wizara inaendelea na mchakato wa upimaji mashamba ya Serikali pamoja na ufuatiliaji wa hati miliki katika maeneo ya mabonde ya mpunga ya Bandamaji, Koani na Mchangani. Pia maeneo

ya Kisakasaka, Cheju, Bumbwisudi, Mtwango, Hanyegwa mchana, Pangeni na mashamba yote ya misitu na mpira tayari yamekabidhiwa ZIPA.

4 TZS 3,160,544,622 zimekusanywa kuanzia Julai, 2021 hadi Machi, 2022.

48. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, imeidhinishiwa jumla ya TZS 2.4 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.82 bilioni ni mishahara na TZS 542.63 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 programu imepata jumla ya TZS 1.4 Bilioni sawa na asilimia 58 (TZS 1.11 bilioni ni Mishahara na TZS 279.1 milioni kwa matumizi mengineyo).

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

49. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Programu imetekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

a. Mapitio ya Sera ya Kilimo yamekamilika kwa ngazi ya Wizara; Sheria ya Minazi, Sheria ya Mbegu na Sheria ya Viuatilifu na Uhifadhi wa Mimea zimekamilika na kupitiaTume ya Kurekebisha Sheria zinaendelea na ukusanyaji wa maoni ya wadau;

b. Mapitio ya Mpango Mkakati wa Mboga na Matunda (Horticultural Strategic Plan) yamefanyika kwa kushirikiana na Mradi wa Agri-connect. Aidha, kwa kushirikiana na UWAMWIMA Mpango Mkakati wa Kilimo Hai

wa Zanzibar umeandaliwa;

c. Andiko la kazi ya Kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ya Wilaya limekamilika, na kuanza kwa utoaji wa mafunzo ya utayarishaji mpango;

d. Kuratibu na kushiriki katika Kongamano la Kitaifa la Viungo lililofanyika – Misali Sunset Beach Hoteli Pemba, ambalo limehudhuriwa na washiriki zaidi ya 150.

e. Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wameandaa taarifa za Wilaya za Sensa ya Kilimo ya Mwaka 2019/2020. Aidha, ripoti ya Sensa ya Kilimo ya Zanzibar inatarajiwa kutoka hivi karibuni.

f. Kikao cha Mashirikiano baina ya Wizara ya Mifugo ya SMT na Wizara ya Kilimo Zanzibar kilifanyika Maktaba Chakechake Pemba tarehe 28-29 Novemba, 2021 na kuhudhuriwa na wataalamu 40 wa Zanzibar na Tanzania Bara. Lengo ni kuangalia changamoto na fursa zilizopo katika sekta ya mifugo ili kuweka maazimio ya kutatua changamoto hizo na kutumia fursa kwa njia ya mashirikiano Pemba.

50. Mheshimiwa Spika, programu ndogo ya Mipango iliidhinishiwa jumla ya TZS 612.2 milioni kwa kazi za kawaida (TZS 328.6 milioni ikiwa ni mishahara na TZS 283.5 matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 programu imepata jumla ya TZS 169.3 milioni sawa na asilimia 28 (TZS. 135.2 milioni mishahara, TZS.34.0 milioni matumizi mengineyo.

Programu Ndogo ya Uratibu naUtekelezaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili na Mifugo Pemba

51. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya sekta ya Kilimo, Maliasili na Mifugo. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango ya Wizara ya Kilimo Maliasili na Mifugo.

52. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ilitekeleza shabaha zifuatazo:

1. Afisi imefanikisha ziara na vikao vinne kwa Kamati ya Biashara, Kilimo na Utalii, Kamati ya PAC na Kamati ya Bajeti katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;

2. Vikao vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na Idara na Taasisi mtambuka za sekta ya kilimo-Pemba vilifanyika;

3. Ziara za wageni na viongozi wa Wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za Wizara pamoja na kuhudhuria katika sherehe na kumbukumbu za kitaifa Unguja na Pemba;

4. Mashirikiano na taasisi nyenginezo (Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii) yameimarishwa.

53. Mheshimiwa Spika, Programu ndogo ya uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Programu hii iliidhinishiwa TZS 3.93 bilioni (TZS 3.64 bilioni mishahara na TZS 284.8 milioni ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Programu

imepata jumla ya TZS 2.39 bilioni sawa na asilimia 61 (TZS 2.15 bilioni ni Mishahara na TZS 241.8 milioni kwa kazi za kawaida.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Makadirio ya Mapato

54. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS 4.70 bilioni kupitia vianzio vyake 11 viliopo Unguja na Pemba. **(Kiambatanisho Nam. 3C)**

Makadirio ya Matumizi 2022/2023

55. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 53.590 bilioni kati ya fedha hizo jumla ya TZS 23.243 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 11.887 bilioni Mishahara na TZS 4.765 bilioni matumizi mengineyo). Aidha, jumla ya TZS 6.596 bilioni ikiwa ni Ruzuku (TZS 3.645 bilioni Mishahara na TZS 2.951 bilioni matumizi mengineyo), kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo **(Kiambatanisho Nam. 4D).**

56. Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa jumla ya TZS 30.342 bilioni (TZS 21.647 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 8.694 bilioni kutoka SMZ). **(Kiambatanisho Nam. 4D).**

57. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake nne kuu kama ifuatavyo:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu
3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo

58. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara pia itaendelea na utekelezaji wa Miradi mitatu (3) ya Maendeleo inayoendelea ambayo ni Mradi wa kudhibiti Sumu Kuvu (TANIPAC), Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na Mradi wa kudhibiti Nzi wa Matunda. Vilevile, Wizara itatekeleza Miradi miwili Mipya ambayo ni Kupunguza Upotevu wa Mazao na Mradi wa Kuendeleza na Kuhifadhi Miti ya Asili inayotoweka-**"Mradi wa Kurejeshea Msitu wa Kijani" (Kiambatisho Nam. 4B na 4C).**

MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

59. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Wizara ya Kilimo, Uwagiliaji, Maliasili na Mifugo itatekeleza Malengo yafuatayo:

1) Kujenga miundombinu ya umwagiliaji hekta 370 na kuunga umeme wa njia kubwa bonde la Cheju B.
2) Kuendelea kuhamasisha kilimo biashara katika mazao ya mboga, matunda na viungo kwa kutumia teknolojia za kisasa, ili kuongeza uzalishaji wenye tija na uhifadhi wa mazingira.
3) Kuanzisha miradi midogo itakayopelekea kuongeza kipato kwa WAKALA wa Matrekta ikiwemo; kituo cha mafunzo ya udereva, eneo la kuoshea magari na Kutengeneza zana ndogo za kilimo na kuziuza kwa wakulima.
4) Kukamilisha ujenzi wa maghala mawili (2) ya hifadhi ya chakula yatakayohifadhi tani 2000 kila moja.
5) Kuotesha miti hekta 130 (hekta 100 Mashamba Serikali 30 Mikoko), na kuhamasisha jamii kupanda hekta 300 na kutoa huduma mashamba ya Serikali.
6) Kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi kufikia 100,000 kupitia miradi ya uekezaji ya Hifadhi za Misitu.
7) Kutoa chanjo ya maradhi ya miripuko kwa

ng'ombe 30,000; kuku 200,000 na mbwa 8,000 pamoja na kupandisha ng'ombe 2,000 kwa njia ya sindano

8) Kuimarisha huduma za ugani kwa kuwapatia ushauri wafugaji 13,000 Unguja na Pemba.
9) Kufanya tafiti saba mpya (4 Unguja na 3 Pemba) na kuendeleza tafiti zinazoendelea sita (4 Unguja na 2 Pemba) za kilimo na maliasili; pamoja na tafiti za kutatua changamoto za kijamii mbili na kuimarisha miundombinu ya utafiti;
10) Kuendelea na utoaji wa maslahi ya wafanyakazi 1,050 ikiwemo ubani (120) likizo (860), muda wa ziada (60) na kusaidia matibabu (10).
11) Kukamilisha mapitio ya Sheria 2 (Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999 na Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu Nam. 10 ya 1996).
12) Kutayarisha Mpango Mkakati wa Uzalishaji wa Mifugo, Mkakati wa kuimarisha zao la karafuu na uzalishaji wa mazao ya Viungo nchini, pamoja na kukamilisha Mipango ya Sekta ya Kilimo ya Kiwilaya; na
13) Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu za Sekta ya Kilimo.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO

60. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina programu ndogo mbili:

i. Kuendeleza miundombinu ya Umwagiliaji maji
ii. Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula

61. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa jumla ya TZS 34.087 bilioni kati ya hizo TZS 6.358 bilioni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 4.482 bilioni Mshahara, TZS 1.875 bilioni kwa matumizi mengineyo). TZS 5.231 bilioni ni Ruzuku (TZS 3.013 bilioni Mshahara na TZS 2.217 bilioni kwa matumizi mengineyo) kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Aidha, programu inaombewa TZS 22.497 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (TZS 21.647 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 850.00 milioni kutoka SMZ).

Programu Ndogo ya Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji

Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Uimarishaji na Usimamizi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji kwa Mwaka 2022/2023

a. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 370 katika bonde la Cheju B pamoja na ujengaji wa misingi ya ndani (Tertiary canals) kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Cheju na Mlemele.

b. Uungaji wa umeme wa njia kuu (3-phase) kwa visima 15 katika bonde la Cheju B pamoja na

kumalizia uungaji wa umeme huo katika bonde la Kibokwa na Kilombero;

c. Uwekaji sawa wa konde katika bonde la Mlemele pamoja na ujengaji wa viungio (structures) katika misingi ya umwagiliaji maji (irrigation canals) pamoja na misingi wa kutolea maji ya ziada (drainage canals).

d. Kufanya ukarabati na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji na kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalamu juu ya usimamizi na uendeshaji wa skimu pamoja na kushajiisha wakulima kuchangia gharama;

e. Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakao athirika wakati wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa miundombinu.

62. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu ndogo hii inaombewa **TZS 22.103 bilioni** ambapo TZS 1.603 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.053 bilioni Mshahara na **TZS 550.482 milioni** kwa matumizi mengineyo). Vilevile, programu inaombewa **TZS 20.500 bilioni** kwa kazi za maendeleo ambapo TZS 20.000 bilioni kutoka kwa wahisani EXIM BANK ya Korea na TZS. 500.000 milioni kutoka SMZ.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.

Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula Mwaka 2022/2023

- **a.** Kufuatilia uzalishaji wa mpunga katika eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na Unguja 13,000);
- **b.** Kuotesha miche 300,000 ya minazi (200,000 Unguja na 100,000 Pemba); mikarafuu 500,000 (300,000 Pemba na 200,000 Unguja) na miti ya matunda 300,000.
- **c.** Kununua na kusambaza mitego 100,000, lita 200 za dawa ya kunasia nzi waharibifu wa matunda na lita 60 za dawa ya kuulia nzi waharibifu wa matunda;
- **d.** Kukagua mazao ya kilimo yanayoingia na kusafirishwa nje ya nchi ikiwemo karafuu.
- **e.** Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi 50 watendaji wa Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula na wa muda mrefu 5 katika nyanja mbalimbali;
- **f.** Kuwapatia mafunzo mabwana/mabibishamba 200 juu ya mbinu mchanganyiko za udhibiti wa viumbe waharibifu wa mimeapamoja na matumizi bora ya viwatilifu;
- **g.** Kuandaa aina 4 ya vitini kwa ajili ya kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji wa minazi, mazao ya viungo, wadudu waharibifu wa nzi wa matunda na viwavi vamizi (fall armyworm);
- **h.** Kununua pikipiki na vitendeakazi kwa ajili ya watendaji;
- **i.** Kuweka mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

63. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 11.983 bilioni** ambapo TZS 4.754 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 3.429 bilioni Mshahara na TZS 1.325 bilioni kwa matumizi mengineyo).Vilevile, programu inaombewa ruzuku ya TZS 5.231 Bilioni (TZS 3.013 ikiwa ni mishahara na TZS. 2.217 Bilioni matumizi mengineyo kwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar. Aidha, Wizara inaombewa jumla ya TZS 1.997 bilioni fedha za maendeleo (TZS 350.000 milioni kutoka SMZ na TZS 1.647 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

64. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inatekelezwa chini ya Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.

Shabaha Zitakazotekelezwa na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa Mwaka 2022/2023

a. Kuendeleza utoaji wa huduma za matengenezo ya matrekta na zana za kilimo za Serikali na sekta binafsi pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi, vipuri na vilainishaji; na

b. Kuanzisha miradi midogo midogo itakayopelekea kuongeza kipato kwa WAKALA, ikiwemo: kituo cha mafunzo ya udereva, kutengeneza eneo la kuosha magari, kuanzisha kituo cha ufundi wa magari, umeme, welding na uchomaji na kutengeneza zana ndogo ndogo za kilimo na kuziuza kwa wakulima.

65. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inaombewa jumla ya **TZS. 2.464 bilioni** kwa ajili ya ruzuku (TZS 846.500 milioni Mshahara, TZS 1.617 bilioni kwa matumizi mengineyo).

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar – ZARI

66. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo – ZARI inatekelezwa chini ya Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula,

Shabaha zitakazotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar –ZARI kwa mwaka 2022/2023

67. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi ya Utafiti inalenga kutekeleza yafuatayo:

1. Kuendeleza tafiti za zamani 6 (4 Unguja na 2 Pemba) pamoja na Kufanya tafiti mpya 4 za kilimo na maliasili zifuatazo:

a) Matumizi ya Mwani kwa mbolea katika Migomba,

b) Kuendeleza zao la Mpunga wa juu aina ya NERICA 1,
c) Kufanya utafiti wa kukusanya aina ya viumbe hai (fauna species diversity),
d) Kuangalia mafanikio ya matumizi ya mbolea ya UDP kwenye Mahindi na Alizeti;

2. Kuimarisha miundombinu ya utafiti ikiwemo ujenzi wa "Screen house mbili na Greenhouse mbili"

3. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 50 na muda mrefu saba (7) katika ngazi za Shahada ya kwanza (4), uzamili (2) na uzamivu (1).

4. Kulifufua shamba la matunda Mndo na

5. Kuzalisha miche bora na salama ya matunda na viungo.

68. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo – ZARI, inaombewa jumla ya TZS 2.767 bilioni ikiwa ni ruzuku (TZS 2.167 bilioni Mshahara na TZS 600.200 milioni kwa matumizi mengineyo).

PL0102 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

69. Mheshimiwa Spika, Programu hii inayo programu ndogo moja ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Misitu

Shabaha zitakazotekelezwa na programu ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu

70. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- **a.** Kuotesha miche 1,000,000, kujenga miundombinu ya vitalu 3 pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji wa vitalu;
- **b.** Kupanda miti hekta 130 (hekta 100 Mashamba Serikali na 30 Mikoko), pamoja na kuhamasisha jamii kupanda hekta 300 na kutoa huduma mashamba ya Serikali;
- **c.** Kuzifanyia tathmini (COFMA) Misitu 22 ya Jamii, kuzikamilisha 8 na kuhamasisha jamii matumizi ya nishati na mbinu mbadala. Pamoja na kuanzisha cofma mpya 8 (Unguja 4 na Pemba 4) ambazo utaratibu wake wa awali umeshaanza;
- **d.** Kuhakiki mipaka ya mashamba (4) ya Serikali, vitalu vya kuotesha miti na Misitu ya Hifadhi (5) ya Unguja Pemba kwa ajili ya kuzipatia hati za kisheria;
- **e.** Kufanya tathmini, kuanzisha, kupitia kanuni na Kuhakiki Mipaka kwa ya mashamba na Msitu ya Hifadhi
- **f.** Kufanya tafiti za miradi mbadala kwa jamii, wanyapori adimu ndani ya Hifadhi na kutoa huduma kwa wanyamapori waliopo mazizi ya Serikali; na
- **g.** Kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi kufikia 100,000 kupitia miradi ya uekezaji wa mashirikiano katika maeneo ya Hifadhi za Misitu.
- **h.** Kuimarisha ulinzi katika Hifadhi za Misitu ya Jamii kwa kufanya doria 500 Unguja na Pemba.

71. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Misitu inaombewa jumla ya **TZS 4.059 bilioni** ambapo (TZS 2.459 bilioni Mshahara na TZS 600.664 milioni kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu imeombewa TZS 1.00 Bilioni kutoka SMZ kwa ajili ya Mradi wa Uhifadhi Miti ya Asili na Adimu inayotoweka. **(Kiambatisho Nam 4D)**

PL0103 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

72. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina programu ndogo moja ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI)

Programu Ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo

Shabaha zitakazotekelezwa na Programu hii 2022/2023

73. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

- **a.** Kupandisha ng'ombe 2,000 (Unguja 1,200, na Pemba 800) kwa njia ya sindano.
- **b.** Kuimarisha malisho kwa kupanda malisho ekari 10 katika shamba la malisho Kizimbani.
- **c.** Kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya mifugo kwa kutoa mafunzo kwa wafugaji juu ya ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi na kuku.

d. Kuwatembelea wafugaji 12,000 (8,000 na Pemba 4,000) na kuwapa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji.

e. Kuchanja kuku 200,000 dhidi ya ugonjwa wa mahepe, gumboro na ndui, Mbwa 8,000 (Unguja 5,000 na Pemba 3,000) dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa (Rabies) na Ng'ombe 30,000 dhidi ya magonjwa chambavu, kimeta ugonjwa wa ngozi na ugonjwa wa miguu na midomo;

f. Kufunga uzazi wanyama 200 (mbwa 50 na paka 150) ili kupunguza tatizo la wanyama wazururaji.

g. Kutoa huduma ya maabara ya mifugo kwa uchunguzi wa maradhi mbali mbali ya mifugo.

74. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu hii inaombewa jumla ya TZS 9.271 bilioni ambapo kati ya hizo TZS 2.907 Bilioni ni kwa matumizi ya kawaida (TZS 2.157 bilioni mshahara na TZS 749.398 milioni matumizi mengineyo). Vilevile, Wizara inaombewa fedha za ruzuku TZS. 2.164 Bilioni kwa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na TZS 5.00 bilioni fedha za maendeleo kutoka SMZ.

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI

75. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI inatekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Mifugo

Shabaha Zitakazotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ZALIRI 2022/2023

76. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu hii itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kuendeleza tafiti tatu 3 zinazoendelea na kufanya tafiti 3 mpya zifuatazo:
   a) Tathmini ya usafi wa Maziwa kwa wafugaji,
   b) Tathmini ya Ufanisi wa Malisho na
   c) Tathmini ya Kuku wa Nyama wanaochinjwa katika umri tofauti);

2. Kukamilisha ujenzi wa jengo la kiwanda cha chakula cha kuku, maabara, pamoja na ujenzi wa mabanda matatu ya utafiti wa Ng'ombe, Mbuzi na Sungura pamoja na ofisi Pemba.

3. Uendelezaji wa mashamba ya malisho ekari 10 (Chamanangwe 6 na Kizimbani 4);

4. Utayarishaji wa kanuni za Utafiti;

5. Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Taasisi Kizimbani ikiwemo (Ofisi, Banda la Utafiti wa ng'ombe, banda la mbuzi, Ukarabati wa Maabara, jengo la kiwanda cha chakula cha Mifugo na Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano).

77. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu ya ZALIRI inaombewa TZS 2.164 bilioni (TZS 631.300 milioni Mshahara na TZS 733.300 milioni kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS 800.000

Milioni fedha za maendeleo kutoka SMZ kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Taasisi.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO

78. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina programu ndogo tatu:

i. Utawala na Uendeshaji
ii. Mipango, Sera na Tafiti
iii. Uratibu wa kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Pemba

79. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo inaombewa jumla ya TZS 6.171 bilioni ambapo kati ya hizo TZS 2.787 bilioni mishahara na TZS 1.539 matumizi mengineyo. Aidha, programu inaombewa TZS 1.844 Bilioni kutoka SMZ kwa Mradi wa Kupunguza athari ya Upotevu wa Mazao.

Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji

Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji 2022/2023

80. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, huduma hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a. Kuendelea na utoaji wa maslahi ya wafanyakazi 1,050 kwa ufanisi ikiwemo ubani (120) likizo (860), muda wa ziada (60) na kusaidia matibabu (10).

b. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

c. Kusimamia na kudhibiti mali za Serikali kwa upimaji wa hati miliki katika maeneo ya mabonde ya mpunga ya Bandamaji, Koani na Mchangani.

81. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo inaombewa jumla ya TZS 3.216 bilioni ambapo (TZS 2.102 bilioni mshahara na TZS 1.113 bilioni kwa matumizi mengineyo).

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

Shabaha Zitakazotekelezwa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2022/2023

82. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a. Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Nam. 11 ya 1999, Mpango Mkakati wa Mboga na Matunda na Mpango Mkakati wa Kilimo Hai;

b. Kukamilisha utayarishaji wa Mipango Mikakati ya Kilimo ya Wilaya na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ZASDP;

c. Kufanya tafiti 2 za kiuchumi na Kijamii kwa mujibu wa Ajenda ya utafiti ya Zanzibar na

kuchapisha matokeo ya tafiti hizo;

d. Kusimamia utekelezaji wa Mradi na progarmu zote za Wizara;

e. Kuendelea kusimamia Mpango Mkakati wa Takwimu;

f. Kuendeleza mashirikiano na taasisi za ndani, kikanda na kimataifa.

83. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya TZS 2.955 bilioni ambapo (TZS 685.301 milioni ikiwa ni mishahara na TZS. 425.482 milioni kwa matumizi mengineyo), Aidha, programu inaombewa TZS 1.844 bilioni fedha za Maendeleo kutoka SMZ kwa ajili ya Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao).

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

84. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 4.700 bilioni** kupitia vianzio 11 viliopo Unguja na Pemba.

85. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 53.590 bilioni** ambapo **TZS 23.248 bilioni** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 11.887 bilioni Mishahara na TZS 4.765

bilioni matumizi mengineyo). **TZS 6.596 bilioni** ikiwa ni Ruzuku (TZS 3.645 bilioni Mishahara na TZS 2.951 bilioni matumizi mengineyo), kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. **Kiambatisho Nam 4D.**

86. Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa jumla ya **TZS 30.341 bilioni** (TZS 8.694 bilioni kutoka SMZ na TZS 21.647 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo).

SHUKURANI

87. Mheshimiwa Spika, baada ya uwasilishaji huo, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili, na mifugo zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ; Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji; Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Wizara ya Kilimo (SMT), Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT), CARI, Wizara ya Maliasili na Utalii (SMT) na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT).

88. Mheshimiwa Spika, Wizara inayashukuru Mashirika binafsi ya ndani, na nje yakiwemo ZSTC, VIUNGO (PDF), TAHA, UWAMWIMA, COSTECH, COMMUNITY FOREST, AFIRI, TALIRI, TPRI, "ZAASO" na "ZSPCA". Tunazishukuru pia nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia kuendeleza sekta hii, zikiwemo Japan, China, Korea ya Kusini, Marekani, UAE, Oman na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo. Benki ya Dunia, Benki ya Tanzania ya Kilimo, Benki ya Maendeleo ya Afrika, ICRAF, IFAD, UNDP, FAO, JICA, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, CFC, WCS, GARC, PASS, "WHO", Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) na Umoja wa nchi za Ulaya - "EU"

89. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa aliyekuwa Waziri wa Kilimo kabla yangu Mhe. Dkt. Sudi Nahoda Hassan kwa kunipa mashirikiano na kunikabidhi majukumu pale ambapo alipoishia. Vilevile, nawashukuru viongozi wa Wizara hii ninayoiongoza wakiwemo; Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini WKUMM, Wakurugenzi wa Maidara na Taasisi za Wizara na watumishi wote kwa juhudi zao, ushirikiano na ushauri walionipatia katika kipindi hiki kifupi jambo ambalo limeniwezesha kusimama hapa leo hii kuwasilisha Hotuba hii ya Bajeti kwa mwaka 2022/2023. Pia nawapongeza kwa dhati wakulima, wafugaji, watunza mazingira na wadau wote wa sekta ya kilimo kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya kilimo ya chakula na biashara pamoja na utunzaji wa misitu nchini.

90. Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru Viongozi Wateule wote wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Wakulima, Wafugaji na Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu, Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

91. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS
WAZIRI, WIZARA YA KILIMO,
UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO
ZANZIBAR

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1A na 1B: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2020 -2021 – Zanzibar

Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2020 -2021 - Zanzibar				
ZAO	2020		2021	
	Eneo lililopandwa (Ekari)	Uzalishaji (Tani)	Eneo lililopandwa (Ekari)	Uzalishaji (Tani)
Muhogo	26,996	158,465	30,949	181,668
Mpunga	32,995	40,328	28,172	30,353
Migomba	7,772	66,840	7,104	61,094
V/vikuu	582	2,912	1,549	7,746
Majimbi	1,153	4,404	1,148	4,386
J/kunde	2,752	1,376	2,233	1,117
V/Vidogo	8,183	57,284	5,259	36,813
Mtama	428	163	367	139
N/nyasa	642	308	775	372
Mahindi	3,815	1,907	3,256	1,628
Mbaazi	1,173	3,787	497	1,606
Uwele	206	41	201	40
Maboga	648	3,072	297	1,407
Chooko	478	191	314	126
Mboga na Matunda	13,083	54,935	16,470	64,820
Jumla	**100,907**	**396,014**	**98,591**	**393,315**

Kiambatisho 1B: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2020 - 2021



Kiambatisho 1C: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchimjwa, 2021



Kiambatisho 1D: Uzalishaji wa Mayai na Maziwa 2021



Kiambatisho 1E: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2020 na 2021



Kiambatanisho Nam. 2A:
Jadweli la Upatikanaji wa Mapato Julai 2021 hadi A, 2022

KASMA NAMBA	CHANZO CHA MAPATO	MAKADIRIO 2021/2022	JUMLA	ASILIMIA
OFISI KUU PEMBA				
1422022	ADA YA MAZAO YA MISITU	43,651,000	34,914,900	80
1421001	MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE	1,500,000	2,318,000	155
1422060	MAPATO YA MASHAMBA	196,300,000	279,129,000	142
1422048	ADA UKAGUZI WA MAZAO	27,710,000	29,638,400	107
1421011	UTIBABU WA WANYAMA	13,780,000	15,457,700	112
1422068	MAPATO YA MIFUGO	600,000	430,000	72
1422066	UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI	10,000,000	8,908,500	89
JUMLA PEMBA		**293,541,000**	**370,796,500**	**126**
IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA				
1422022	ADA YA MAZAO YA MISITU	250,000,000	226,237,200	90
1421001	MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE	8,000,000	-	0
1422066	UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI	790,000,000	637,177,524	81
		1,048,000,000	**863,414,724**	**82**
IDARA YA KILIMO				
1422048	ADA UKAGUZI WA MAZAO	100,000,000	107,454,800	107
1422060	MAPATO YA MASHAMBA	-	11,500,000	
		100,000,000	**118,954,800**	**119**
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO				
1423002	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	25,000,000	22,079,200	88
1422060	MAPATO YA MASHAMBA	75,000,000	2,000,000	3
1422066	ADA YA UINGIZAJI WAGENI	20,000,000	8,432,000	42
		120,000,000	**32,511,200**	**27**
IDARA YA MIFUGO				
1421011	UTIBABU WA WANYAMA	2,337,885,000	1,604,675,568	69
1422068	MAPATO YA MIFUGO	574,000	577,000	101
1422060	MAPATO YA MASHAMBA	-	6,000,000	
		2,338,459,000	**1,611,252,568**	**69**
WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO				
1421014	HUDUMA ZA MATREKTA	100,000,000	163,614,830	164
		100,000,000	163,614,830	164
JUMLA UNGUJA		**3,706,459,000**	**2,789,748,122**	**75**
JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA		**4,000,000,000**	**3,160,544,622**	**79**

Kiambatanisho Nam. 2B:

UCHAMBUZI WA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI APRIL, 2022

Program	Makadirio	Mshahara	Matumizi Mengineyo	Ruzuku M/Mengineyo	Ruzuku Mshahara	Maendeleo SMZ	Maendeleo Muhisani	Jumla	Asilimia
PL0101 Maendeleo ya Kilimo	**37,308,868,500**	**2,697,198,000**	**174,207,824**	**847,546,166**	**2,234,185,665**	**2,010,442,017**	**21,276,292,795**	29,239,872,467	78
SL010101 Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji	26,772,192,000	715,493,190	31,049,341	-	-	1,957,442,017	21,164,089,595	23,868,074,143	89
SL010102 Utafiti na Mafunzo ya kilimo-ZARI	2,895,000,000	-	-	80,000,000	1,652,883,715	-		1,732,883,715	60
SL010103 Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula	5,287,576,500	1,981,704,810	143,158,483			53,000,000	112,203,200	2,290,066,493	43
SL010105 Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo	2,354,100,000	-	-	767,546,166	581,301,950	-	-	1,348,848,116	57
PL0102 Maendeleo ya Rasilimali za Misitu	**2,766,841,500**	**1,434,000,465**	**62,463,050**					1,496,463,515	54
SL010201 Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu	*2,766,841,500*	1,434,000,465	62,463,050		-		-	1,496,463,515	54
PL0103 Maendeleo ya Mifugo	**6,681,816,000**	**1,314,703,755**	**60,103,571**	**80,000,000**	**466,138,304**		**-**	1,920,945,630	29
SL010301 Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo	5,290,116,000	1,314,703,755	60,103,571					1,374,807,326	26
SL010303 Taasisi ya Utafiti wa mifugo	1,391,700,000	-	-	80,000,000	466,138,304		-	546,138,304	39
PL0105 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo	**6,947,227,000**	**3,408,199,135**	**555,039,555**	**-**	**-**		**-**	3,963,238,690	57
SL010501 Utawala naUendeshaji wa Kazi za Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na	2,404,731,500	1,119,853,260	279,167,399	-	-		-	1,399,020,659	58
SL010502 Mipango, Sera na Utafiti	612,252,500	135,253,525	34,058,156	-	-		-	169,311,681	28
SL010503 Uratibu Ofisi Kuu Pemba	3,930,243,000	2,153,092,350	241,814,000	-	-	-	-	2,394,906,350	61
JUMLA KUU	**53,704,753,000**	**8,854,101,355**	**851,814,000**	**927,546,166**	**2,700,323,969**	**2,010,442,017**	**21,647,240,000**	**36,991,467,507**	**69**

Kiambatisho Nam. 3A

MRADI WA KUDHIBITI NZI WA MATUNDA

Gharama za mradi kwa mwaka 2021/2022: Mradi uliombewa **TZS.120,000,000** kutoka Shirika la Mionzi Duniani (IAEA) na **TZS. 100,000,000** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2021 fedha zilizopatikana kutoka IAEA ni TZS. 73,707,456 na TZS 53,000,000 kutoka SMZ.

Utekelezaji wa Malengo 2021/2022

i. Kazi ya utengenezaji wa mitego 5,000 ya kunasia nzi wa matunda inaendelea katika Maabara ya wadudu iliyopo Kizimbani.
ii. Ripoti ya tathmini ya maendeleo ya mradi kwa mwaka 2021/22 imeandaliwa na kutumwa IAEA.

Kwa mwaka 2022/2023: Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 748.2 milioni (TZS 350 milioni kutoka Serikalini na TZS 388.240 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo IAEA.)

Malengo kwa mwaka 2022/2023

Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya matumizi ya mbinu mchanganyiko katika maeneo maalumu
ii. Kukusanya takwimu za matunda kwa utaratibu maalum (systematic fruit sampling)
iii. Kununua vifaa vya kukusanyia sampuli za wadudu wa matunda
iv. Kununua vifaa kwa ajili ya kampeni ya nzi wa matunda
v. Uendeshaji na Uratibu wa Mradi

Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kununua vifaa vya kuimarisha mfumo wa uingizaji na utoaji wa mazao
ii. Kununua vifaa vya maabara ya karantini
iii. Kununua vifaa na dawa za kunasia nzi wa matunda
iv. Kufanya ziara za kimafunzo kwa viongozi na watendaji

Kiambatisho Nam. 3B

MRADI WA KUDHIBITI SUMUKUVU TANZANIA (TANIPAC)

Kwa mwaka 2021/2022: Mradi uliombewa **TZS 3,120,468,377** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia. Hadi kufikia Februari, 2022 fedha zilizopatikana ni **TZS 112,,203,200**

Malengo ya Mwaka 2021/2022

1. Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu
2. Ununuzi wa mashine 2 za maabara kwa ajili ya kupima sumukuvu
3. Kufanya uchunguzi wa hali ya sumukuvu hapa Zanzibar
4. Ujenzi wa maghala za kuhifadhi nafaka Unguja moja (1) na Pemba moja (1)
5. Kutoka mafunzo ya uelewa na udhibiti wa Sumukuvu kwa wafanyabiashara Zanzibar
6. Kutoka mafunzo ya kanuni bora kwa wakulima kwa wakulima Zanzibar
7. Kujenga uelewa wa Sumukuvu kwa wawakilishi
8. Kuimarisha usimamizi wa ujenzi wa maghala Unguja na Pemba
9. Utoaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa watekelezaji wa Mradi
10. Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa vihenge vya chuma vya kuhifadhia mazao
11. Kutoa mafunzo kwa waandishi wa habari
12. Kutengeneza vifaa vya kutoa elimu(T-shirt, poster, leaflets nk)

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2021/2022

1. Udhamini wa wanafunzi wawili (2) wa shahada ya uzamili na mmoja (1) wa shahada ya uzamivu unaendelea katika vyuo vya Tanzania.
2. Mashine za kupima sumukvu katika bidhaa za chakula zimenunuliwa na kukabidhiwa katika taasisi ya ZARI na ZFDA. Mashine hizo ni HPLC kwa ZFDA na Evidence Investigator kwa ZARI, pia wataalamu katika taasisi hizo wamepatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mashine hizo.
3. Uchunguzi wa hali ya Sumukuvu (Situational Analysis on Aflatoxin) hapa Zanzibar umekamilika na ripoti kamili imewasilishwa katika ofisi ya Mradi kwa utekelezaji.
4. Maghala ya kuhifadhia nafaka yanaendelea kujengwa katika eneo la Kizimbani Unguja (asilimia 48) na Ole Dodeani Pemba (asilimia 42).
5. Mafunzo ya uelewa na udhibiti wa Sumukuvu kwa wafanyabiashara 200 (Unguja 120 na Pemba 80) yamefanyika.
6. Mafunzo ya siku tatu (3) kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima 30 yametolewa
7. Mafunzo ya uelewa wa Sumukuvu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yamefanyika
8. Kamati mbili (2) zenye wajumbe kutoka ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa na Wizara zimeundwa na kuwezeshwa kufanya usimamizi wa maghala Unguja na Pemba
9. Wawezeshaji wawili kutoka ZFDA na ZBS walihudhuria mafunzo ya wiki moja yaliyowajengea uwezo katika kutoa elimu ya udhibiti wa sumu kuvu
10. Kwa kushirikiana na VETA na Mamalaka ya Ufundi Stadi Zanzibar VTA mradi unaendelea na usajili wa vijana 40 Unguja na Pemba kupitia Mabaraza ya Vijana ya Wilaya kwa ajili ya kuwapa mafunzo hayo

Kwa mwaka 2022/2023: Mradi unaombewa jumla ya **TZS 1,259,028,000** kutoka kwa wafadhili

Malengo kwa mwaka 2022/2023

1. Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu
2. Kuendelea na uimarishaji wa kamati za usimamizi wa ujenzi wa maghala Unguja na Pemba
3. Kuendelea na malipo ya wakandarasi wa ujenzi wa maghala Unguja na Pemba
4. Kuendelea na shughuli za kutoa elimu ya sumukuvu kwa wadau kwa mfano wakulima
5. Kushiriki katika maonesho ya kitaifa
6. Kutengeneza vifaa vya uelimishaji wa jamii k.v vipeperushi mabango kofia na fulana
7. Kununua vifaa kwa ajili ya ghala Unguja na Pemba
8. Usimamizi na uendeshaji wa ofisi
9. Kwa kushirikiana na VETA na Mamalaka ya Ufundi Stadi Zanzibar VTA mradi utaendelea kuwapa mafunzo ya utengenezaji wa vihenge vya chuma kwa vijana 40 Unguja na Pemba

Kiambatisho Nam. 3 C

MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI

Gharama za mradi: Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Mradi huu ulipangiwa **TZS 2.90 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 22.89** bilioni kutoka EXIM BANK ya Korea. Hadi kufikia Aprili 2022 mradi umepata **TZS 1.95 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 21.164 bilioni** kutoka EXIM BANK ya Korea.

Malengo kwa Mwaka 2021/2022

i. Usimamizi na Ufatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji utakaoendeleza hekta 453 katika mabonde ya Cheju, Kilombero na Mlemele. Aidha, kazi za ujenzi wa bwawa la umwagiliaji katika bonde la Mlemele limekamilika.

ii. Ulipaji wa fidia ya mazao kwa wakulima 600 watakaoathirika wakati wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Chaani, Cheju, Kilombero na Mlemele.

iii. Uungaji wa umeme wa njia kuu (3 phase line) katika skimu za umwagiliaji maji za Kilombero, Cheju na Kibokwa.

Utekelezaji wa Malengo

i. Kazi za ujenzi na usimamizi wa mradi wa umwagiliaji maji zinaendelea katika mabonde sita kwa Unguja na Pemba, zikijumuisha ukamilikaji wa mabwawa matatu kwa upande wa Unguja (bwawa la Kinyasini na la Chaani) na upande wa Pemba (bwawa la Mlemele) na kuanza kuhifadhi maji ya umwagiliaji ya maeneo hayo. Kwa upande wa bonde la Mlemele kazi ya uwekaji kifusi umekamilika na kunaendelea na kazi ya ujenzi wa viungio (structures) ya misingi ya umwagiliaji maji pamoja na uwekaji sawa wa konde wa mwisho na kwa upande wa bonde la Cheju kazi inayoendelea ni uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima na uwekaji wa kifusi chenye urefu wa kilomita 16 kwenye njia za mashambani.

ii. Kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ya maji zinaendelea na utekelezaji wake ambao umefikiwa **90%**, kwa upande wa asilimia za utekelezaji kwa kila bonde ni kama ifuatavyo; Kilombero hekta **292** imefikia **(85%),** Mlemele hekta **44** imefikia **(90%)** na Cheju hekta **314** imefikia **(90%).**

iii. Malipo ya fidia ya mazao ya wakulima yamefanyika kwa jumla ya wakulima 325 katika mabonde ya Chaani, Cheju, Kilombero na Mlemele.

iv. Kazi za Uungaji wa umeme wa njia kuu (3 phase line) katika skimu za umwagiliaji maji zinaendelea ambapo zimeanza katika bonde la Cheju na kufikiwa asilimia 80 kwa utekelezaji wake Cheju na kazi hii itaendelea kwa mabonde ya Kilombero na Kibokwa.

SHABAHA ZA 2022/2023

i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 370 katika bonde la Cheju B pamoja na ujengaji wa misingi ya ndani (Tertiary canals) kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani, Cheju na Mlemele.

ii. Uungaji wa umeme wa njia kuu (3-phase) kwa visima 15 katika bonde la Cheju B pamoja na kumalizia uungaji wa umeme huo katika bonde la Kibokwa na Kilombero;

iii. Uwekaji sawa wa konde katika bonde la Mlemele pamoja na ujengaji wa viungio (structures) katika misingi ya umwagiliaji maji (irrigation canals) pamoja na misingi wa kutolea maji ya ziada (drainage canals).

iv. Kufanya ukarabati na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji na kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalamu juu ya usimamizi na uendeshaji wa skimu pamoja na kushajiisha wakulima kuchangia gharama;

v. Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakao athirika wakati wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa miundombinu.

Kiambatisho Nam. 4 A

Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023

KASMA NAMBA	CHANZO CHA MAPATO	MAKADIRIO 2022/2023
OFISI KUU PEMBA		
1422022	Ada Ya MazaoYa Misitu	45,560,732
1421001	MauzoYa Uzalishaji Wa Miche	1,565,625
1422060	MapatoYa Mashamba	150,000,000
1422048	Ada Ukaguzi Wa Mazao	28,922,313
1421011	Utibabu Wa Wanyama	14,382,875
1422068	MapatoYa Mifugo	626,250
1422066	Uingizaji Wa Wageni Ngezi	10,437,500
JUMLA PEMBA		**251,495,295**
IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA		**1,338,466,000**
1422022	Ada Ya MazaoYa Misitu	293,750,000
1421001	MauzoYa Uzalishaji Wa Miche	8,350,000
1422066	Uingizaji Wa Wageni Jozani	1,036,366,267
IDARA YA KILIMO		**146,024,400**
1422048	Ada Ukaguzi Wa Mazao	134,024,400
	Mapato ya Mashamba	12,000,000
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO		**135,000,000**
1423002	Mauzaji Ya Mazao Na Miche	25,000,000
1422060	MapatoYa Mashamba	90,000,000
1422066	Ada Ya Uingizaji Wageni	20,000,000
IDARA YA MIFUGO		**2,583,591,793**
1421011	Utibabu WaWanyama	2,576,992,680
1422068	MapatoYa Mifugo	599,113
	Mapato ya Mashamba	6,000,000
WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO		**245,422,245**
1421014	Huduma Za Matrekta	245,422,245
JUMLA UNGUJA4		**4,448,504,705**
JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA		**4,700,000,000**

Kiambatisho Nam 4B

MRADI WA KUPUNGUZA UPOTEVU WA MAZAO YA KILIMO

Huu ni mradi mpya : Kwa mwaka 2022/2023 Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 1,844,847,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - SMZ
Lengo kuu la Mradi: Kupunguza Upotevu wa Mazao ya Kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula kwa Wilaya 10 za Zanzibar (Wilaya 6 Unguja na Wilaya 4 Pemba). Lengo hili linajumuisha kuwawezesha wakulima kupata masoko baada ya mavuno na kuwapatia mashine za kuchakata mazao kwa kuongeza thamani na kipato kwa wakulima wa mazao ya kilimo.
Malengo Makhsusi ya Mradi vi. Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za upotevu wa mazao ya kilimo; vii. Kuboresha uwezo wa taaluma kwa kupunguza athari za upotevu wa mazao ya kilimo; **viii.** Kuwezesha mfumo wa masoko ya kilimo ili kuboresha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.
Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali i. kufanya utafiti wa awali ili kupata taarifa za msingi za upotevu wa mazao ii. kuanzisha mfumo wa taarifa za upotevu wa mazao ya kilimo iii. Kuendesha mafunzo juu ya mbinu bora za utunzaji na uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna iv. Kuandaa ziara za mafunzo kwa wahusika wa mnyororo wa thamani (wakulima, wasindikaji wa mazao, wasafirishaji na wafanyabiashara) ili kujifunza na kuhamasishwa katika utunzaji wa mazao v. Kuwawezesha wakulima kwa kuwapatia vifaa vya kuchakata mazao ya kilimo kwa wilaya za Unguja na Pemba.

Kiambatisho Nam 4C

MRADI WA KUREJESHA URITHI WA KIJANI

Huu ni mradi mpya : Kwa mwaka 2022/2023 Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 1,000,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ.
Lengo kuu la Mradi: kuendeleza urithi wa kijani wa Zanzibar kwa uzalishaji wa miche ya misitu na matunda na upandaji katika maeneo ya wazi ya mashamba ya serikali, maeneo yaliyoathirika na uchimba wa maliasili zisizorejesheka na maeneo ya misitu ya jamii
Malengo Makhsusi ya Mradi • Kuotesha miche bora angalu 700,000 kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitano • Kutayarisha Maeneo na kupanda miti hekta 275 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano. • Kuimarisha miundombinu katika vitalu vya serikali unguja na pemba vya uzalishaji wa miche • Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uoteshaji wa miche na upandaji kila mwaka.
Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali a) Ununuzi na upatikanaji wa vifaa, mbegu, Mbolea na dawa kwa ajili ya kuoteshea miche b) Kusimamia uotesha miche katika vitalu sita (6) c) Kuajiri vibarua wa muda kwa kipindi cha miezi mitatu d) Kuandaa mpango wa upandaji pamoja na Usimamizi wa miti iliyopandwa e) Kutayarisha maeneo kwa ajili ya kupanda miti f) Kusafirisha miche kwenda maeneo ya upandaji g) Uhamasishaji wa jamii katika upandaji wa miti h) Kufanya ukarabati wa majengo na ofisi ziliopo katika Vitalu i) Ukarabati wa mabanda, ya miundombinu ya vitalu j) Kurekebisha miundombinu ya maji na umeme katika vitalu k) Ununuzi wa vyombo vya usafiri (Lori 2, na Pikipiki 6) l) Uendeshaji wa program kwa uandaaji wa ripoti na usimamizi wa rasilimali fedha,watu (Mafuta na stationaries) m) Kusimamia na kukagua Miti iliyopandwa na kumea (Survival percentage) n) Urejeshaji wa miti iliyokufa (Replanting) o) Kuajiri vibarua wa muda kwa Upaliliaji wa miti iliopandwa na kumea

Kiambatanisho Nam. 4D: MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU KWA MWAKA 2022/2023							
Program	**Makadirio**	**Mshahara**	**Matumizi Mengineyo**	**Ruzuku M/Mengineyo**	**Ruzuku Mshahara**	**Maendeleo SMZ**	**Maendeleo Muhisani**
PL0101 Maendeleo ya Kilimo	**34,087,822,000**	**4,482,818,000**	**1,875,964,000**	**2,217,900,000**	**3,013,900,000**	**850,000,000**	**21,647,240,000**
PL0102 Maendeleo ya Misitu	**4,059,674,000**	**2,459,010,000**	**600,664,000**	**-**	**-**	**1,000,000,000**	
PL0103 Maendeleo ya Mifugo	**9,271,607,000**	**2,157,609,000**	**749,398,000**	**733,300,000**	**631,300,000**	**5,000,000,000**	**-**
PL0105 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara	**6,171,684,000**	**2,787,563,000**	**1,539,274,000**	**-**	**-**	**1,844,847,000**	**-**
JUMLA KUU	**53,590,787,000**	**11,887,000,000**	**4,765,300,000**	**2,951,200,000**	**3,645,200,000**	**8,694,847,000**	**21,647,240,000**

MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU KWA MWAKA 2022/2023